JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

SHULE YA SEKONDARI NKOWE

Namba za simu

Mkuu wa shule- 0684420004

Makamu mkuu wa shule-0683081454

Mwalimu wa malezi: 0783141575

Mkuu wa Shule
S.L.P. 76,
RUANGWA

Tarehe: …….

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ----------

S.L.P----------

YAH: MAAGIZO YA MASHARTI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NKOWE MWAKA 2020/2021

Hongera!

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (V) katika shule ya sekondari Nkowe. Anatakiwa kuripoti hapa shuleni tarehe ----------.Akichelewa wiki mbili baada ya tarehe ya kufungua shule atakuwa amepoteza nafasi yake na itachukuliwa na mtu mwingine kama ilivyotangazwa.

MAHALI SHULE ILIPO

Shule hii ni ya bweni na ipo Kijiji cha MPUMBE,wilayani Ruangwa mkoa wa Lindi. Usafiri kwa watakaotoka Njia ya Dar es Salaam kuna mabasi yanatoka DSM hadi Ruangwa moja kwa moja wanatakiwa kupandia kituo cha mabasi cha Temeke(sudani) au Mbagala rangi 3 watashuka kijiji cha Mpumbe, ndipo shule ilipo. Kwa watakaotokea njia ya Songea kuna magari yanatoka Songea lindi/ songea mtwara watashuka kijiji kinaitwa Nanganga kisha watapanda daladala zinazoelekea Ruangwa kisha watashuka kijiji kinachoitwa Mpumbe watakuwa wameshafika shuleni si mbali kutoka Mpumbe kijijini ni kama mita 750

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ambazo unatakiwa kuzisoma kwa makini nakuzifanyia kazi.

(i) Fomu ya kupimwa afya ya Mwanafunzi kutoka kwenye Hospitali inayotambulika na Serikali.
(ii) Fomu ya mahitaji muhimu ya shule
(iii) Fomu za sheria za shule
(iv) Mkataba wa Mwanafunzi wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
(v) Fomu ya habari za Mwanafunzi na Mzazi
(vi) Tamko la mzazi kukubaliana na sheria na kanuni za shule.

Shule itafunguliwa tarehe……..Nafasi yako itatunzwa mpaka tarehe .....ambapo ndiyo tarehe ya mwisho ya kuripoti shuleni. Hivyo kamilisha mahitaji mapema na kuwahi shule kabla nafasi yako haijajazwa na mtu mwingine endapo utachelewa.

NB: Unatakiwa kuja na**Leaving Certificate,Result Slip, Cheti cha kuzaliwa na picha (passport size2)**

Nakutakia maandalizi mema na safari njema ya kuja hapa shuleni :

KARIBU SANA.

“EDUCATION FOR PROGRESSIVE DEVELOPMENT”

.....

CHACHA MWITA

MKUU WA SHULE

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

1. **Karo na Michango ya Shule.**

(a) Karo ya shule ni**Tshs. 70,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa yote kwa wakati mmoja au Tshs.35,000/= kwa muhula, kila mwanzo wa muhula.

NB: Karo na michango mingine ya shule ilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. 71101100098 NMB (Nkowe Secondary School Recurrent Account) na kisha kuwasilisha **bank pay slip** siku utakayoripoti shuleni na iandikwe majina kamili ya mwanafunzi husika

(b) **Michango mingine inayotakiwa kulipwa Shuleni**

- Fedha ya Tahadhari ni Tshs. 5,000/=(haitarejeshwa)
- Mchango wa ukarabati ni Tshs. 15,000/=
- Fedha ya Taaluma Tshs 20,000/= kwa mwaka
- Fedha ya Ulinzi Tshs. 10,000/= kwa mwaka
- Fedha kwa ajili ya Kitambulisho Tshs. 6500/=
- Fedha kwa ajili ya T-shirt yenye nembo ya shule Tshs.13,500/= ambayo itavaliwa kama sare kwa siku za Juma tano na Ijumaa.
- Fedha kwa ajili ya mpishi 12,000/=
- Kujiunga na mfuko wa CHF kwa matibabu ya ndani ya wilaya Tshs 6,000/= kwa wale tu wasiokuwa na bima ya NHIF
- Mchango wa mfuko wa matibabu ya dharula Tshs 6,000/= ambao utatumika kuwasafirisha wanafunzi wanapohitaji matibabu ya dharula kwenda Hospitali ya Wilaya.

2. **Sare za Shule kwa wavulana.**

a) Suruali mbili (2) za Gray colour **(rangi ya kijivu iliyokolea**) zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo .
b) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu na yenye kola shingoni.
c) Viatu vya ngozi jozi (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda
d) Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)
e) Nguo za michezo, bukta moja na jezi yake rangi ya zambarau, Track suit nyekundu na viatu vya michezo.
f) Aje na sweta moja (1) rangi ya kijivu (**gray colour**) liwe la kufuma. V- shape
g) Suruali mbili (2) za damu ya mzee **(maroon colour**) shamba dress zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo .

3. **Sare za Shule kwa wasichana**

a) Sketi (2) za Gray colour **(rangi ya kijivu iliyoiva**) zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo (mshono uwe v-shape).
b) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mirefu na yenye kola shingoni au nusu kanzu kwa wale tu wanaovaa hijabu.
c) Viatu vya ngozi jozi (2) viatu visiwe na urembo wowote na wala visiwe vya kupanda

d) Soksi imara nyeusi jozi mbili (2)
e) Nguo za michezo Track suit nyekundu na viatu vya michezo.
f) Aje na sweta moja (1) rangi ya kijivu (**gray colour**) liwe la kufuma. V- shape
g) gauni (2) za damu ya mzee **(maroon colour**) shamba dress zenye urefu na upana wa heshima na zilizoshonwa kwa unadhifu na sio kwa mapambo .
h) baibui nyeusi kwa waislamu kuendea msikiti tu

NB: Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare zilizoanishwa hapo juu muda wote, na hata awapo safarini na haruhusiwi kuja na nguo yoyote ya nyumbani na haruhusiwi kusuka au kuwa na nywele ndefu.

4. **Mahitaji kwa ajili ya malazi**
(a) Godoro la sponji moja 2½, x 6''
(b) Shuka mbili (2) za rangi ya bluu bahari iliyoiva
(c) Chandarua chenye dawa kwa ajili ya kujikinga na Mbu wanaoambukiza malaria.
(d) Mto na foronya yake
(e) Taulo moja
(f) Sanduku la chuma (bati) linalofungwa na kufuli.
4. **Mahitaji kwa ajili ya chakula**
(a) Sahani (b) Bakuli (c) Kikombe (d) Kijiko

5.**Mahitaji kwa ajili ya Taaluma.**

Ream moja (1) ya karatasi za photocopy (A4) zitakazobadhiwa siku ya kuripoti shuleni, Daftari za kutosha kulingana na masomo yako, Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (CBG au PCB),Dissecting kit, Scientific calculator na kalamu ya wino wa blue au mweusi na kalamu ya risasi au penseli.

6. **Vifaa vya Usafi**
(a) Fyekeo (b)Panga (c)Jembe (d) Fagio laini (e)Sqeeser /Mopper (1)
(f) Ndoo kwa matumizi yake (g) Fagio ngumu la chooni(1)dawa ya chooni lita 3,(h) Reki

SHERIA ZA SHULE

1. Wanafunzi wasimame na kusalimia mwalimu au mtu yeyote anayewazidi umri anapopita au anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano
2. Wanafunzi wampokee mizigo mwalimu au mtu yeyote anayewazidi umri anapopita karibu yao
3. Wanafunzi waheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wao
4. Ni mwiko mwanafunzi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yao, kwa mwalimu, watumishi wasiowalimu, au viongozi wa serikali ya wanafunzi na watu wengine
5. Wanafunzi waheshimiane na kusaidiana wao kwa wao
6. Wanafunzi wapende kujitumna na kuheshimu kazi zote

7. Wanafunzi watii kengele ya shule pindi inapogongwa kwa kukimbilia eneo husika
8. Wanafunzi waheshimu bendera ya taifa, wimbo wa taifa na bendera ya taifa inapopandishwa au kushushwa
9. Ni mwiko kwa wanafunzi kufanya mambo yafuatato;-
   (i) Kufuga kucha ndefu
   (ii) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
   (iii) Kupigana
   (iv) Kuongeza mapambo juu ya sare ya shule kama vile kuvaa bangili, heleni, shanga n.k
   (v) kupaka rangi ya kucha na macho (wanja)
   (vi) kukata nyusi
   (vii) kutia dawa nywele
   (viii) kukata nywele panki
   (ix) kukaribisha au kupokea wageni nje ya utaratibu wa shule
10. wanafunzi waheshimu ofisi zote za shule
11. wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo ;-
   (i) Jiko la shule isipokuwa kwa mwnafunzi aliyeko zamu au ruhusa maalumu
   (ii) Nyumba za Walimu na wafanya kazi wengine mpaka kwa kibali
   (iii) Nyumba za kufikia wageni(guest houses)
   (iv) Vilabu vya pombe
   (v) Majumba ya starehe
12. Wanafunzi waonyeshe heshima wawapo kwenye kumbi za mikutano na chakula
13. Wawpo darasani wanyooshe mikono juu na wasimame wanapojiubu na kuuliz maswali
14. Wanafunzi wwahudhurie vipindi vyote vya darasanai na kazi za mikono pindi zinapotolewa
15. Wanafunzi wafanye bidii katika masomo yao. Ni mwiko kupata alama chini ya 50% katika somo lolote
16. Wanafunzi wahudhulie mikutano ya shule kama vile baraza la shule, kupandisha bendera ya taifa , mikutano ya darasani na bweni
17. Wanafunzi waendapo likizo warudi shuleni kwa tarehe zilizopangwa
18. wanafunzi wavae sare za shule wakati wote wa;-
   a. Masomo darasani
   b. Kusafiri kwenda rikizo na kurudi
   c. Safari za shule
   d. Kwenda hospitali
   e. Mhadhara wa shule ikiwa ni pamoja na baraza la shule
19. Wanafunzi nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

a) Wizi
b) Kumpa au kupata mimba au kuharibu mimba ndani nan je ya shule
c) Utoro

d) Ulevi wa aina yeyote na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bagi, cocaine, mirungi n.k
e) Uesharati.uhusiano wa jinsimoja,kuoa au kuolewa
f) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
g) Kugoma na kuhamasisha mgomo
h) Kutaka kujiua
i) Kutokuwepo shuleni kwa muda wa miezi mitatu mfululizo bila taarifa
j) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
k) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote
l) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
m) kudharau bendera ya Taifa
n) kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
o) kusuka au kufuga nywele ndefu
p) Kufuga ndevu
q) kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sharia za nchi
r) Kutembelea nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni (GUEST HOUSE)

TAARIFA BINAFSI KUHUSU MWANAFUNZI
(Form hii ijazwe na irudishwe shuleni)

1.Jina la Mwanafunzi……kidato cha ……
2.Kabila la Mwanafunzi……
3. (a) Tarehe na mwaka wa Kuzaliwa …….....Wilaya alikozaliwa mwanafunzi……na Mkoa…….
4.Dini ya mwanafunzi……na tatizo la mwanafunzi kiafya……
5.Jina la kamili la baba……..
Anuani kamili…….....simu……na kazi yake……
6.Jina kamili la mama…….
Anuani kamili…….simu……na kazi yake…….
7.Jina kamili la mtu/mlezi anayemhudumia mwanafunzi ka ada na vitu vingine ……
8. Uhusiano wa mwanafunzi na mlezi……
Anuani kamili…….simu……kazi yake……

9.Orodha ya ndugu aliozaliwanao mwanafunzi, wakianza na wa kwanza kuzaliwa

NA	**JINA**	**UMRI**	**KAZI/MWANAFUNZI**	**KITUO CHA KAZI/SHULE**

12. Baba na mama wanaishi pamoja/wametengana (kata isiyohusika)

13. Uwepo wa wazazi: Baba YUPO/HAYUPO kama amefariki lini…….
Mama YUPO/HAYUPO kama amefariki lini……..

Majina na picha za watu wasiozidi wanne watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi:-

PICHA	PICHA	PICHA	PICHA
JINA	JINA	JINA	JINA
SIMU	SIMU	SIMU	SIMU

RUANGWA DISTRICT COUNCIL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

THE HEADMASTER,
NKOWE SECONDARY SCHOOL,
PO. BOX 76,
RUANGWA.

DATE……

TO:
The Medical officer
……
……..
……..
Re:
NAME……
……

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for full time course of Secondary education at Nkowe Sec School.

1. Eye sight……..
2. Hearing……
3. Speech……..
4. Venereal diseases…….
5. Neurosis……..
6. Pregnancy for girls only…….

Doctor's Remarks……
……
……

Doctor's Advice……
……
……

Doctor's Name……..
Signature……Rubber stamp
Date……

AHADI YA MZAZI/ MLEZI

Mimi…….ambaye ni mzazi wa……..
Aliyetoka shule ya……wilayani……mkoa wa……
Nimesoma na nimeyaelewa maagizo ya kujiunga na shule hii na ninaahidi kuwa nitajitahidi kulipa ada na kumpa mahitaji mengine mwanangu aliyetajwa hapo juu hadi atakapomaliza ELIMU YA SEKONDARI
Sahihi…….Tarehe…….
.

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi…….wa kidato cha ……..
Nmesoma na kuzielewa sharia za shule na naahidi kuzitii na kuzitimiza taratibu zote zilizowekwa.
Sahihi……..
Tarehe……..

…….
MKUU WA SHULE